**BUNGE LA 13 | KIPINDI CHA 4**
**SENETI**

# KWA KANUNI YA MSWADA WA KATIBA YA KENYA (MAREKEBISHO), 2025 (MISWADA YA SENETI NAMBARI 13 YA 2025)

## MAELEZO YALIYORAHISISHWA YA MSWADA

**Wadhamini:** Kiongozi wa Walio Wengi na Kiongozi wa Walio Wachache katika Seneti

**Aina ya Mswada:** Mswada wa Kawaida

### A. Maelezo kwa ufupi

Mswada wa Katiba ya Kenya (Marekebisho), 2025 unalenga kuufanya ugatuzi kuimarika zaidi. Unapendekeza mabadiliko ya Katiba ili kufafanua kwa uwazi majukumu ya Bunge la Taifa na Seneti. Aidha unaimarisha jinsi sheria zinavyotungwa kwa kuhakikisha kwamba Bunge la Taifa na Seneti inahusika katika kuidhinisha sheria. Mswada huu unaanzisha hatua maalum za kushughulikia sheria za kifedha. Kwa ujumla, mabadiliko haya yanalenga mfumo wenye uwazi, uwajibikaji na ulio na ufanisi zaidi katika ngazi za kitaifa na za kaunti.

### B. Muhtasari wa Vifungu

#### 1. Kuimarisha jukumu la Seneti

Mswada wa Katiba ya Kenya (Marekebisho), 2025 unapendekeza kuipatia Seneti mamlaka zaidi na jukumu kubwa kuhusu jinsi nchi inavyotawaliwa. Kwa sasa, Seneti inahusika pakubwa na sheria zinazoshughulikia masuala ya kaunti. Kupitia kwa mswada huu, Seneti itakuwa ikihusika katika kutunga sheria zote, na sio tu zile zinazohusu serikali za kaunti.

Kadhalika, mbali na kuwakilisha kaunti, Mswada huu unaeleza kwamba Seneti inapaswa kuwakilisha vikundi vyenye maslahi maalum kama vile wanawake, vijana na watu wanaoishi na ulemavu. Hii itahakikisha kwamba sauti za Wakenya wote zinasikika katika mchakato wa kutunga sheria.

Badiliko lingine muhimu ni kwamba sasa Seneti itasaidia katika kutayarisha masharti ya kuondolewa kwa maafisa wa serikali na kuidhinisha watu wanaoteuliwa katika nafasi muhimu za umma. Hii inamaanisha kwamba Seneti itakuwa na jukumu thabiti zaidi katika kuhakikisha kwamba maafisa wa umma wanawajibika.

Kadhalika, Mswada huu unaanzisha muundo wazi wa uongozi katika Seneti, kama ule muundo ulio katika Bunge la Taifa. Katika muundo huu mpya, utaratibu wa ukuu katika Seneti utakuwa Spika, Kiongozi wa Walio Wengi, na Kiongozi wa Walio Wachache kwa usanjari huo.

**Hatua hii ina umuhimu gani?**

Hatua ya kuimarisha Seneti ni muhimu sana kwa sababu inaleta uwiano bora baina ya Bunge la Taifa na Seneti. Kwa sasa, maamuzi mengi muhimu, hususan kuhusu fedha na sheria za kitaifa, hutungiwa katika Bunge la Taifa. Hali hii husababisha kaunti na Wakenya wa kawaida kukosa uwakilishi wa kutosha kwenye maamuzi ya kitaifa.

Kwa kuipatia Seneti jukumu thabiti zaidi, Mswada huu unahakikisha kuwa kila kaunti ina sauti imara katika Bunge. Maseneta wanaowakilisha kaunti sasa watahusika katika kutunga sheria zote na kuidhinisha maafisa wa ngazi za juu serikalini na kuamua jinsi fedha zinavyogawanywa na kutumika katika nchi nzima. Hii inamaanisha kwamba kutakuwa na uwajibikaji zaidi katika maamuzi ya serikali, ugavi wa haki wa rasilmali baina ya serikali kuu na serikali za kaunti, ulinzi bora wa kaunti na ugatuzi na uangalizi bora wa maafisa wa umma ili kuhakikisha kwamba wanawahudumia wananchi na wakati wasipofanya hivyo, kwamba kuna taratibu wazi za kuwaondoa mamlakani.

Kwa maelezo rahisi, wakati Seneti inapokuwa na nguvu zaidi, kaunti zitakuwa na uwezo bora wa kutoa huduma muhimu kwa Wakenya wote.

**2. Kufanyia mabadiliko jinsi sheria zinavyotungwa**

Mswada huu unabadilisha jinsi sheria zinavyotungwa nchini Kenya. Kwa sasa, baadhi ya sheria zinaweza kuwasilishwa katika Bunge moja na mara nyingi kuna ukosefu wa makubaliano kuhusu ni Bunge lipi lina maamuzi ya mwisho.

Mswada huu mpya unaruhusu Miswada kuanza ama katika Bunge la Taifa au Seneti, isipokuwa sheria za kukusanya ushuru au mapato, ambayo bado itaanzia kwenye Bunge la Taifa na baada ya hapo kushughulikiwa na Seneti. Badiliko hili linapatia Bunge la Taifa na Seneti jukumu sawa na la haki ya kutunga sheria.

Aidha, Mswada huu unaondoa Ibara ya 110 na ya 114, ambazo awali zilileta mtafaruku kuhusu Miswada ipi iliathiri kaunti na iwapo Seneti ingehusika katika kupitisha Miswada fulani. Kwa kuondoa Ibara hizo, mchakato wa kutunga sheria unakuwa wazi, wa haraka na wenye haki zaidi. Inavyopendekezwa sasa, wakati Mswada unapopitishwa kwenye Bunge moja, lazima utumwe kwa Bunge lile lingine ili kuhakikiwa na kuidhinishwa. Lazima pawe na makubaliano baina ya Bunge la Taifa na Seneti kabla ya Mswada kuwasilishwa kwa Rais ili kupata kibali. Iwapo kuna ukosefu wa makubaliano, mchakato wa usuluhishi utatumiwa ili kupata suluhu.

Kadhalika, Mswada huu unapatia Bunge (Bunge la Taifa na Seneti) jukumu la pamoja katika kushughulikia maoni ya Rais mswada unaporejeshwa ili kushughulikiwa tena.

**Hatua hii ina umuhimu gani?**

Mabadiliko haya yanapunguza mgogoro baina ya Bunge la Taifa na Seneti, ambao umekuwa tatizo hapo awali. Kadhalika, yanafanya mchakato wa kutunga sheria kuwa na ufanisi na wenye kuheshimu dhamira ya Katiba ya kuwa na Bunge la Taifa na Seneti.

Kupitia kwa mageuzi haya—

- hakuna Bunge litakalotawala Bunge jingine;
- sheria zitatungwa kwa mashauriano na ushirikiano; na
- mchakato utakuwa wazi zaidi na rahisi kueleweka.

Mabadiliko haya yatapatia umma imani kwamba Bunge la Taifa na Seneti inafanya kazi kwa pamoja ili kupitisha sheria zinazoshughulikia mahitaji halisi katika nchi nzima.

### 3. Kuendeleza Uwazi, Ushirikiano na Bunge lenye Nguvu zaidi

Mswada huu unaleta mageuzi ili kusaidia kufafanua majukumu ya Bunge la Taifa na ya Seneti, kupunguza migogoro na kuimarisha jinsi Bunge linavyofanya kazi kwa ujumla. Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na ukosefu wa maelewano baina ya Bunge la Taifa na Seneti, hasa kuhusu ni Miswada ipi itahusisha Seneti, jinsi sheria za fedha zinavyopitishwa, na nani ana mamlaka ya mwisho katika michakato fulani. Migogoro hii imeishia katika michakato ya mahakama ya muda mrefu, wakati mwingine ikichelewesha utungaji wa sheria na kudhoofisha utendakazi wa kijumla wa Bunge.

Mswada huu unapendekeza—

- kuondoa sheria zisizo wazi ambazo zimeleta mwingiliano au mkanganyiko (kama Ibara ya 110 na ya 114);
- kuboresha jinsi Miswada inavyopaswa kuwasilishwa, kujadiliwa, kurekebishwa na kuidhinishwa;
- kuonyesha hatua wazi za kushughulikia kibali cha Rais, ikiwa ni pamoja na muda; na
- kuimarisha mchakato wa maridhiano, ili wakati Bunge la Taifa na Seneti zinapokosa kukubaliana kuhusu Mswada, kuna njia iliyowekwa ya kuushughulikia.

**Hatua hii ina umuhimu gani?**

Bunge linapofanya kazi kwa njia bora, huwa sheria zinapitishwa kwa wakati, rasilmali zinagawanywa kwa njia ya haki na mahitaji ya Wakenya yanashughulikiwa kwa ufanisi.
Marekebisho haya yanalisaidia Bunge—

- kuepuka migogoro isiyofaa;
- kufanya kazi kwa utaratibu na kwa heshima baina ya Bunge la Taifa na Seneti;
- kulenga zaidi katika kuhudumia umma na wala sio kujadili kuhusu mambo ya kiufundi; na
- kuimarisha uaminifu kwa kuonyesha umoja na uwazi katika kutunga sheria.

Mabadiliko haya yanalisaidia Bunge kufanya kazi kama chombo kimoja chenye nguvu na ushirikiano katika kutunga sheria zilizo wazi, zenye haki na za kiwakati kwa faida ya Wakenya wote.

### 4. Mchakato wa Bajeti na Uangalizi

Mswada huu unafanya mabadiliko muhimu katika jinsi bajeti ya kitaifa inavyotayarishwa, kujadiliwa na kuidhinishwa. Kwa wakati huu, Bunge la Taifa lina jukumu kubwa kwenye mchakato wa kutayarisha bajeti huku Seneti ikiwa na nafasi finyu, hata ingawa kaunti zinategemea fedha hizo katika kuwahudumia wananchi.

Mswada huu mpya unaruhusu Seneti na Bunge la Taifa kushiriki katika kuhakiki na kuidhinisha bajeti ya kitaifa, makadirio ya mapato na matumizi yake, sheria za kugawa na za kuidhinisha matumizi, zinazoamua jinsi fedha zinavyogawanywa na kutumika. Mswada huu unaondoa sheria za zamani zilizolifanya Bunge la Taifa kuwa mwamuzi wa mwisho kuhusiana na fedha za umma.

Kwa mujibu wa Ibara ya 249(3) ya Katiba, Bunge linahitaji kugawa fedha za kutosha kwa kila tume na ofisi huru ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao. Kadhalika, inataja kwamba bajeti ya kila tume na ofisi huru sharti ziwasilishwe kama mgao tenge ili kuzipatia utambuzi na ulinzi asasi hizi katika mchakato wa bajeti ya kitaifa. Pamoja na sheria hii, hali ilivyo sasa imeiacha Seneti nje katika kuhakiki na kuidhinisha makadiro ya bajeti na miswada ya kuidhinisha matumizi, hata katika hali ambapo Seneti inawajibu wa kikatiba wa kusimamia asasi husika.

Mswada huu unashughulikia pengo hili kwa urasmi kwa kuihusha Seneti katika mchakato wote wa bajeti. Hii inajumuisha uhakiki wa makadirio, ushiriki wa umma, mapendekezo ya kamati na kupitisha sheria za kuidhinisha matumizi. Kwa kufanya hivyo, Mswada huu unasawazisha Ibara ya 221 na ya 249(3) na kuhakikisha kwamba Bunge la Taifa na Seneti, kwa kufanya kazi kwa pamoja, zinatekeleza wajibu wao kamilifu katika usimamizi wa fedha za umma.

Aidha, ushiriki wa Seneti unaleta mtazamo mpana, wenye uwakilishi zaidi kwenye utayarishaji wa bajeti, hasa kuhusiana na mambo yanayogusia ugatuzi na asasi zenye wajibu katika ngazi zote mbili za serikali. Unahakikisha kuwepo kwa uwazi zaidi, uwajibikaji na mwambatano na kaida za kikatiba, ukiwemo usawa na ujumuishaji katika ugavi wa rasilmali. Kusawazisha mchakato huu hauimarishi tu jukumu la Bunge kama chombo kimoja, bali inatekeleza Ibara ya 249(3) kwa njia inayoonyesha dhamira ya ngazi mbili za bunge na kuheshimu asasi huru.

Isitoshe, endapo kuna ucheleweshwaji katika kupitisha sheria zinazoruhusu fedha kugawanywa kwa kaunti, Mswada huu unaliruhusu Bunge kuidhinisha upataji wa kimuda wa fedha ili kaunti ziweze kuendeleza huduma zao za kimsingi.

**Hatua hii ina umuhimu gani?**

Pesa ni uwezo, na jinsi zinavyogawanywa huathiri Wakenya wote. Mabadiliko haya yanamaanisha kwamba—

- kaunti hazitasubiri tena au kutatizika kupata fedha kwa sababu ya kucheleweshwa katika Bunge;
- Seneti sasa itasaidia katika kulinda mgao wenu wa ugatuzi wa kaunti;
- kutakuwa na udhibiti zaidi ili kuhakikisha kwamba fedha hazitumiwi vibaya; na
- ni sharti Bunge la Taifa na Seneti kusikiliza umma wakati wa kuhakiki makadirio ya bajeti.

Mageuzi haya yanahakikisha kwamba pesa zako zinapangiwa vyema zaidi, zinasimamiwa vyema zaidi na zinalindwa vyema zaidi katika kiwango cha kitaifa na cha kaunti yako.

## 5. Kuimarishwa kwa Kaunti

Mswada huu unapendekeza mabadiliko makuu ya kuimarisha kaunti, kuzifanya kuwa huru zaidi na ziwe na uwezo bora wa kuwahudumia wananchi wao. Mojawapo ya mapendekezo

makuu ni kuundwa kwa Hazina ya Bunge la Kaunti katika kila kaunti. Hazina hii itasaidia katika utawala na shughuli za kila siku za bunge la kaunti, ikiwemo kulipa wafanyakazi, kuendesha ofisi, na kutekeleza majukumu ya uangalizi.

Kwa sasa, mabunge mengi ya kaunti hutegemea mamlaka kuu ya kaunti (magavana) ili kupata fedha. Hii inaweza kusababisha ucheleweshwaji, usumbufu, au shinikizo kwa wajumbe wa mabunge ya kaunti. Kupitia Hazina hii mpya, mabunge ya kaunti yatapokea fedha zao moja kwa moja, jambo linaloyafanya kuwa huru zaidi na kuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yao bila woga au mapendeleo.

Kila bunge la kaunti litahitajika kupitisha sheria yake kuhusu jinsi Hazina hiyo itakavyosimamiwa na kutumika. Fedha hizo zitatoka kwa mgao wa mapato ya taifa kwa kaunti, na zikiidhinishwa, zitatolewa moja kwa moja, kumaanisha kuwa hazitaweza kuzuiwa na mamlaka kuu ya kaunti.

**Hatua hii ina umuhimu gani?**

Kaunti imara zinahitaji mabunge ya kaunti yaliyo imara na huru. Mabadiliko haya yanamaanisha kwamba—

- Mabunge ya kaunti yataweza kufanya uangalizi kwa ufanisi zaidi;
- Wajumbe wa mabunge ya kaunti wataweza kufanya kazi bila vizuizi, jambo litakalosaidia kupambana na ufisadi na matumizi mabaya ya fedha;
- kaunti zitaitikia kwa haraka zaidi mahitaji ya wenyeji na kutoa huduma bora; na
- kanuni ya mgawanyo wa madaraka itaheshimiwa katika ngazi ya kaunti.

Mabadiliko haya yanasaidia kulinda sauti ya wananchi katika ngazi ya kieneo kwa kuyafanya mabunge ya kaunti kuwa huru kifedha, yenye uwazi na yenye ufanisi.

## 6. Idhini ya Pamoja ya Maafisa wa Serikali

Mswada huu unapendekeza kwamba uidhinishaji na uangalizi wa maafisa wakuu wa umma ufanywe kwa pamoja na Bunge la Taifa na Seneti, badala ya Bunge moja pekee. Hii inamaanisha kuwa Bunge litafanya kazi kama taasisi moja iliyoungana wakati wa kuchunguza na kuidhinisha uteuzi fulani wa ngazi za juu. Mabadiliko haya yatatumika kwa nyadhifa zifuatazo—

- Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma;
- Mdhibiti wa Bajeti;
- Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Umma;
- Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Umma;
- Mwenyekiti wa Tume ya Ugavi wa Mapato;
- Wenyekiti na makamishna wa tume nyingine za kikatiba.

Katika mabadiliko yaliyopendekezwa, jukumu la kuondoa maafisa hawa, kwa kuzingatia misingi ya kikatiba kama vile utovu wa nidhamu, kushindwa kutekeleza majukumu, au kupoteza uaminifu wa umma, kwa pamoja limepewa Bunge la Taifa na Seneti.

**Hatua hii ina umuhimu gani?**

Mabadiliko haya yanahakikisha kuwa Bunge la Taifa na Seneti inashiriki katika maamuzi muhimu ya kitaifa. Huchochea mashauriano mapana, hukuza maafikiano na huonyesha kanuni ya mfumo wa Bunge la Taifa na Seneti. Kupitia uchunguzi wa pamoja—

- kutakuwa na maoni yenye uwiano kote nchini;
- watu walioteuliwa watakuwa kutoka kote nchini na wenye mitazamo mbalimbali;
- jukumu la Bunge kwa ujumla litaimarishwa na kuunganishwa; na
- taasisi zitapata uhalali mkubwa zaidi kupitia michakato jumuishi.

Kushirikiana katika jukumu hili kwa Bunge la Taifa na Seneti huhakikisha kwamba uteuzi wa ofisi za juu za umma unazingatiwa kutoka mtazamo wa kitaifa na wa kieneo na hivyo basi kusaidia kujenga serikali yenye uwajibikaji zaidi na inayowakilisha wananchi wote.

## C. Hitimisho

Mswada wa Katiba ya Kenya (Marekebisho), 2025 unapendekeza mabadiliko muhimu kuhusu jinsi sheria zinavyoundwa na jinsi mamlaka yanavyogawanywa kati ya Bunge la Taifa na Seneti. Huruhusu Miswada mingi, isipokuwa ile inayohusiana na ukusanyaji wa mapato ya taifa, kuwasilishwa katika Bunge lolote kati ya Bunge la Taifa na Seneti. Hii inamaanisha kwamba Mabunge yote mawili sasa yatakuwa na nafasi iliyo sawa zaidi katika kuunda sheria na kusimamia shughuli za serikali. Mswada huu pia unaipa Seneti jukumu kubwa zaidi katika kufanya maamuzi kuhusu bajeti ya taifa, jinsi fedha zinavyogawanywa kati ya serikali kuu na serikali za kaunti na katika kuidhinisha maafisa wakuu wa serikali. Hii inaunda mfumo wa utawala ulio na uwiano na haki zaidi.

Mswada huu pia unahakikisha kwamba Mabunge yote mawili yanashiriki jukumu sawa katika masuala ya kifedha. Unaondoa kanuni za zamani zilizoipa Bunge la Taifa mamlaka makubwa zaidi kuhusu bajeti ya taifa na matumizi ya fedha. Kwa kubadilisha jinsi Miswada ya kifedha inavyoshughulikiwa, ikiwemo jinsi bajeti zinavyoandaliwa na jinsi maoni ya Rais yanavyoshughulikiwa, Mswada huu unafanya Bunge lifanye kazi kama chombo kimoja. Mabadiliko haya yanaipa Seneti mamlaka halisi katika jinsi fedha zinavyokusanywa, kugawanywa na kutumika kote nchini, jambo linaloleta uangalizi bora zaidi na uwajibikaji.

Kadhalika, yanaboresha jinsi maafisa wakuu wa umma wanavyoteuliwa. Nafasi kama vile Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Umma, Mdhibiti wa Bajeti, na wenyekiti na makamishna wa tume muhimu, sasa zitaidhinishwa na Bunge la Taifa na Seneti. Hii inasaidia kulinda uhuru wa ofisi hizi na kuimarisha imani ya umma katika mchakato huo.

Ili kusaidia ugatuzi, Mswada huu unaanzisha Hazina ya Bunge la Kaunti katika kila kaunti. Hazina hii itasaidia mabunge ya kaunti kusimamia shughuli zao za kila siku na kutekeleza majukumu yao kwa uhuru. Inahakikisha kwamba wajumbe wa mabunge ya kaunti wanaweza kufanya kazi bila kutegemea sana mamlaka tekelezi ya kaunti na hivyo kufanya serikali za kaunti ziwe na uwajibikaji na ufanisi zaidi.

Hatimaye, Mswada huu unaondoa mkanganyiko kuhusu majukumu ya Bunge la Taifa na Seneti katika mchakato wa uundaji sheria. Unabainisha jinsi miswada inavyopaswa kupelekwa kati

ya Mabunge hayo wawili, jinsi usuluhishi unavyopaswa kufanyika iwapo kutakuwa na mgogoro na jinsi Rais anavyopaswa kutoa kibali. Mabadiliko haya yanalenga kupunguza migogoro na kukuza ushirikiano katika Bunge na hivyo kuunda mfumo wa kutunga sheria ulio imara na unaoyashughulikia mahitaji kwa haraka.

## D. Kinachotarajiwa Kutoka Kwako

Kama raia, sauti yako ni muhimu. Mswada huu unapendekeza mabadiliko yatakayoathiri jinsi nchi yetu inavyotawaliwa, kuanzia jinsi sheria zinavyoundwa, jinsi fedha za umma zinavyotumika, hadi jinsi serikali za kaunti zinavyofanya kazi.

Unaombwa usome na uelewe mabadiliko yaliyopendekezwa, uulize maswali pale huelewi, na utoe maoni yako ya dhati. Iwapo unaunga mkono mabadiliko haya, unayapinga, au una mapendekezo ya kuboresha, maoni yako ni muhimu sana. Tafadhali hudhuria mikutano ya umma, wasilisha maoni yako kwa njia ya maandishi, shiriki katika majadiliano ya kijamii, au ushiriki kupitia majukwaa ya mtandaoni na mitandao ya kijamii. Kama mwananchi, una haki ya kuathiri Katiba.

Maoni yako yatasaidia kuimarisha demokrasia yetu.